BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI NA MOJA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Ishirini na Nne – Tarehe 03 Juni, 2026

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua Zitasomwa.

## I. MASWALI:

### Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

115. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ:

Mnamo tarehe 03/03/2026 mwezi 13 Ramadhani, wameonekana Askari wa Idara Maalumu wakipita eneo la wafanyabiashara wadogo Darajani wakiwatisha na kuwakamata wengine. Katika kipindi kama hicho cha mwezi wa Ramadhani, ilizoeleka zamani kuwa wafanyabiashara ndogo ndogo wanapewa nafasi angalau kwa kipindi cha mwezi wa Ramadhani tu, kufanya biashara zao na kupata riziki na baadae wanaondoshwa utaratibu ambao hivi sasa haupo.

(a) Kwa nini Mamlaka zisitumie busara na ubinaadamu wa kuwaacha wafanyabiashara ndogo ndogo kufanya biashara zao kwa kipindi cha mwezi wa Ramadhani tu na ukimalizika wawaondoshe kama ilivyokuwa ikifanyika zamani.

(b) Kwa nini zinatumika nguvu wakati mwengine kupitiliza katika kuwadhibiti wafanyabishara ambao hawana hata silaha.

353. MHESHIMIWA SEIF HAMAD SULEIMAN (Jimbo la Ole) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Hivi karibuni tumeshuhudia masoko ya Jumbi na Kwanyanya yamejaa maji kutokana na mvua zilizonyesha.

(a) Je, kuna tafiti gani iliyofanyanyika mpaka kupelekea kujengwa masoko katika maeneo ambayo yanajulikana yana asili ya kuingia maji.

(b) Kwa kuwa masoko haya yanaingia maji, je, ni ipi thamani ya fedha (Value for Money) iliyopatikana.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

359. MHESHIMIWA SEIF HAMAD SULEIMAN (Jimbo la Ole) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa kuwa Vyuo Vikuu na Vyuo vya Elimu ya Kati vinasimamiwa na *TCU* na *NACTVET* ambavyo sivyo vyombo vya Muungano;

(a) Je, ni ipi mipaka ya *TCU* na *NACTVET* kwa Zanzibar.

(b) Je, Wazanzibari wananufaika vipi na tozo zinazotozwa na TCU na *NACTVET* hapa Zanzibar.

383. MHESHIMIWA DKT. MAHMOUD OMAR HAMAD (Jimbo la Tumbatu) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Ni upi mpango wa Serikali wa ukarabati wa Skuli Kongwe za Msingi na Sekondari ambapo baadhi yao zinaonekana kuvuja na kubomoka.

**Wizara ya Afya:**

161. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Je, Serikali inachukua hatua gani kudhibiti magonjwa ya mripuko na yasiyoambukiza kama kisukari, shindikizo la damu na ugonjwa wa selimundu “sickle cells anemia”.

**Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo:**

73. MHESHIMIWA MAHFOUDH ABDALLA MOHAMMED (Jimbo Magomeni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo:

Mnamo miaka ya 90 kulikuwa na mashindano maarufu sana ya *juvenile, junior na central* Taifa, ambayo yalikuwa yanasimamiwa na viongozi wa Kamati ya *Central League* kama vile marehemu Said Ali, Kocha Juma, kocha Chua, kocha Dulla Sande, Mwalim Hamis Mussa na wengineo. Mashindano hayo yaliibua vipaji vya vijana wengi kama vile Nadir Kanavaro, Abdi Babi, Makame Vigema, Simai Golo, Jeba na wengineo wengi.

Je, ni sababu zipi zilizofanya programu zile za vijana kupoteza msisimko na kupelekea Zanzibar kupungua uzalishaji wa wachezaji wenye vipaji halisia vya soka.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

486. MHESHIMIWA SHAFI MOHAMMED SHAFI (Jimbo la Wete) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Wananchi wenye mashamba yao ambayo yanatumika kwa ajili ya kuchimbwa jiwe na mchanga, wamekuwa kwenye wakati mgumu na kujiuliza maswali yasiyo na majibu kuhusiana na upande wa Serikali kuchukuwa asilimia 70 na mwenye shamba akapewa asilimia 30.

(a) Kwa kiasi gani wananchi hao wanakosea kwa kuiona Wizara inawakandamiza wananchi wenye mashamba.

(b) Kwa nini Serikali isichukuwe hiyo asilimia 30 na mwananchi wakampa asilimia 70.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

117. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Hivi karibuni, Wizara ilitutangazia kuwa kuna mradi wa kugawa ng’ombe 257 kwa Unguja na Pemba wataotumika katika kupata maziwa ambayo yatagaiwa kwa watoto wa skuli za Unguja na Pemba.

(a) Je, mradi huo unafadhiliwa na nani, ni wa muda au utakuwa endelevu.

(b) Je, utaratibu utakuwa vipi wa kugawa maziwa hayo kwa skuli za Unguja na Pemba.

(c) Je, ng'ombe hao watagaiwa kwa watu au taasisi zipi kusimamia, na gharama za uendelezaji zitatolewa na nani

**Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi:**

152. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Je, ni kwa kiasi gani Sheria za Usalama Barabarani zinazingatiwa na ni hatua gani zinachukuliwa kwa wanaozikiuka sheria hizo.

178. MHESHIMIWA MAHMOUD SHINENI ALI (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Serikali kupitia Shirika la Bandari Zanzibar (ZPC) limefanya ukarabati katika Bandari ya Abiria ya Malindi, Unguja.

(a) Ni gharama za kiasi gani zimetumika katika ukarabati huo.

(b) Ni kampuni gani ilipatiwa zabuni ya kufanya ukarabati wa Bandari hiyo na kwa utaratibu gani.

(c) Kwa nini Serikali inaendelea na ukarabati na kutumia mabilioni ya pesa za umma huku kukiwa na Mradi wa Ujenzi wa Bandari Mpya ya Abiria ya Mpiga Duri.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

223. MHESHIMIWA MAKAME MOHAMED SUFIANI (Jimbo la Chumbuni) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Katika eneo la Mnara wa Kumbukumbu ya vifaa vya dunia, inaonekana kutengeneza maduka na majengo ambayo yamekaa bila ya kutumika kwa zaidi ya mwaka.

Je, Wizara yako ina mpango gani wa kuanza kutumika eneo hilo ambalo limepoteza mamilioni ya fedha za umma.

**<u>Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:</u>**

305. MHESHIMIWA JUMA USONGE HAMAD (Jimbo la Chaani) – Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Tunaishukuru Sekali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa utekelezaji wa ajenda ya Uchumi wa Buluu (Blue Economy). Katika kuitekeleza ajenda hiyo, wanawake wengi wa Pwani Mchangani na Kandwi wamehamasika katika kilimo cha mwani ingawa wanakabiliwa na changamoto ya athari za mvua hasa ikizingatiwa kuwa sasa tunaelekea katika msimu huo.

(a) Je, Serikali kupitia Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi ina mpango gani wa kujenga makaushio ya mwani katika shehia ya Pwani Mchangani.

(b) Ni wakulima wangapi wa jimbo la Chaani wamepatiwa nyezo mbalimbali katika kilimo hiki cha mwani.

## II. <u>HOJA ZA SERIKALI:</u>

**<u>Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:</u>**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kwa mwaka 2026/2027.

**Zanzibar,**
**03 Juni, 2026.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA LA**
**<u>WAWAKILISHI, ZANZIBAR</u>**